

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LAMU EAST  
CONSTITUENCY –KIUNGA, HELD AT MSISINI**

**ON**

**FRIDAY 3<sup>RD</sup> MAY, 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LAMU EAST – KIUNGA CONSTITUENCY, ON**  
**FRIDAY 3<sup>RD</sup> MAY, 2002**

**PRESENT**

**Com. Dr. Mosonik arap Korir**  
**Com. Mr. Ahmed I Hassan**

**Secretariat in attendance:**

|               |   |                           |
|---------------|---|---------------------------|
| Treza Apondi  | - | Programme Officer         |
| Carolly Okeyo | - | Asst. Programme Officer   |
| David         | - | Sign Language Interpreter |
| Asha Boru     | - | Verbatim Recorder         |

**Meeting started at 10.15 a.m. chaired by Com. Mosonik arap Korir**

**Com. Mosonik:** Sasa ningependa kwanza, kuwasalimia sehemu ya uwakilishi bungeni ya Lamu Mashariki Kiunga. Sisi tumetoka Nairobi kutoka Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya, Tumekuja siku ya leo kuyasikiza maoni yenu ama mapendekezo yenu kuhusu Katiba ya Kenya vile ingerekebishwa, kabla yakuanza kabisa pengine tumuombe mtu moja atuombee halafu tuendelee, nani anaweza kutuombea leo?

Maombi kwa lugha ya Kiarabu.

Asante sana nitasimama kidogo halafu baadaye nitaketi tukiwa tunaendelea na mkutano nilisema kwamba sisi tumetoka Tume

ya Kurekebisha Katiba ya Kenya pengine mmejua ya kwamba Makamishena wa Tume ni watu ishirini na tisa. Wakati huu sisi sote tuko Mkao wa Pwani, tumegawanyika kwa vikundi vikundi vya watu watatu, wanen wawili kama sasa pengine tukiwa leo hapa wengine wako Mwatate, Taveta, Matuga, Changamwe, Garsen, Magarini na Bahari na wanaendelea na mikutano kama huu wetu wa leo.

Niwajulishe kwanza kwa wenzangu wafanyi kazi wa Tume kwanza kwa mkono wangu wa kulia niko na Kamishna hapa mwenzangu anaitwa Ahmed Issak Hassan,

**Com. Hassan:** Assalam Aleykum,

**Com. Mosok:** halafu kuna wengine, moja huyu ameketi hapa anaitwa Treza Apondi yeye anaitwa Programme Officer –

**Treza Apondi:** Assalam Aleykum

**Com. Mosonik:** Halafu karibu naye ni Bw. Okeyo ambaye ni Asst. Programme Officer

**Caroly Okeyo:** Assalam Aleykum, upande ule mwengine kuna Asha Mohamed (Boru) ambaye anarekodi nitawaeleza baadaye vile anarekodi anaitwa Verbatim Recorder, halafu hapa kuna Mr. Muturi ama Bw. Muturi yeye anafanya ile yaku interpret kama mtu hasikii ambaye anaweza kusoma ile yakuonyesha na mkono, pengine kuna mtu ama hakuna ambaye atahitaji, okay, kati kati pale kuna pilot wetu, hawa ni wenzetu wote tume toka kwa Tume na pengine kabla yakuendelea tungempa nafasi Bw. Chief hapa atukaribishe halafu atupatie ruhusa tuendelee.

**Jamal Fankupi:** Makamishna pamoja na timu yenu mlokuja nayo, wazee wa Kiunga, Salaam Aleykum,

Hatuna budi kwanza kuwakaribisha Kiunga ijapokuwa umeona safari ni ya mbali, na pia hamkujali mumeweza kufika ili kuja kusikia maoni ya wananchi wale walioko hapa, katita Division hii. Ni vizuri sana na tumewashukuru sana kwa vile mumeweza kufika nakupata maoni kutoka pembe ya Kenya kabisa, matumaini yangu ni kwamba, maoni yetu yatatiliwa maanani na kuweza kufirikiwa na kuchukuliwa kama vile sehemu zingine ya nchi yetu ya Kenya. Wananchi wa Kiunga, leo hii ni fursa yetu sisi na fursa yetu ya mwisho katika Lamu District na mpaka kufikiwa hapa Kiunga kwa hivyo kile kilichoko ni tutoe ili kiweze kusikiwa na kuweza kuandikwa na kupelekwa pale panapo stahili ili kuweko na urekebishiwa wa Katiba. Kwa hivyo sitokuwa na mengi yakuzungumza bali mengi yatatakikana kutoka kwenu nyinyi, ili pengine zile sehemu zingine hawakuweza kuzungumza juu yetu sisi au jambo linalo tuhusu sisi lakini wenyewe ndio tutakayo weza kujizungumzia, uwanja ni wetu sisi. Musitarajie kwamba Faza amezungumzia issue ambae yaguzia, Kiunga au sehemu nyingine, ikiwa sisi wenyewe hatuwezi kuzungumza na hatutoweza kuzungumza, basi hakuna atakaye weza kutuzungumzia zile shida zetu au vile tunavotaka Katiba ibadilike ki namna gani, kulingana na hapa petu vile tulivo. Kwa hayo machache nasema asanteni sana, tujitokezeni kwa wingi tena kama safari ya

kwanza na tupeane maoni kila moja alikuwa kiu hapa safari ya kwanza yakutaka kuzungumza na wengi wakapewa fursa mpaka wakati ukafika. Kwa hivyo na leo pia iwe ni hivyo hivyo ili hawa mabwana wakiondoka hapa, waondoke na mengi kutoka Kiunga Division. Kwa hayo machache nakomea hapo, na kuwa ambiya tena karibuni Kiunga.

**Com. Mosonik:** Kama Bw. Chief amesema tuko sehemu yenu leo, na jana tulikuwa Faza na baada ya leo tutakuwa tumemaliza na Consitutency yenu. Tutaendelea kwenda Consitutency zote zingine hapa Pwani halafu baadaye mikoa mingine mpaka tumalize na tukimaliza tutaenda Nairobi, tutaandika repoti kuhusu vile nyinyi mulisema na wa Kenya wengine kwa Constitutency halafu mwishowe kutakuwa na mkutano mkuu wa Taifa, ambako tutapata nafasi sisi wote kujadili hayo maoni yenu, na kuandika Katiba mpya ya Kenya.

Bila kupoteza wakati, sasa ningependa kueleza kwamba , tutataka watu watoe maoni, wengi wamejiandikisha kwa kikaratasi hiki, yule ambae anataka kutoa maoni ajiandikishe kwa kikaratasi. Wapi yule Mohamed ambae alikuwa anaandikisha, ye ye ndio anaandikisha wale amba wanataka kutoa maoni, yule Mohamed ambae ni District Coordinator wenu upande huu. Baada yakijiandikisha ukijiandikisha unaonyesha unasema kwa niaba yako wewe mwenyewe mtu binafsi, ama kwa niaba ya kikundi, halafu wale amba hawataki kutoa maoni lakini wako kwa mkutano, tungependa wajijandikishe tena waseme wao ni observers, kwa ajili baadaye tunataka kusema watu namba hii ndio walikuja kuhudhuria mkutano wa Tume sehemu hii.

Halafu kutoa maoni ni njia mbili, unatoa maoni kama umeyaandika hayo maoni tuseme kwa memorandum ama kibarua kidogo ama unatoa tu kwa mdomo. Yule ambae anatoa akiwa ameandika, tutampa kama dakika tano tu, kufafanua yale ameyandika na kuacha hiyo memorandum yake hapa kwa Treza, *ni wewe?* Ya, kumuachia Treza hapa na memorandum ataiacha hapa.

Tutakuwa tunanasa yale yote muliyosema kwa mitambo vile mumeona hapa kuna hiyo cassette na Asha Mohamed (Boru) anayaandika na sisi Makashinas hapa tunaandika. Kamishna mwenzangu leo hajisikii vizuri ndio mimi nitaendesha hii kazi , lakini tunawa hakikishia ya kwamba maoni yote tutayanasa, yule mwenye memorandum dakika tano, asiye na memorandum akichukua muda mrefu sana ni dakika kumi.

Tafadhali tuenze na Famau Ali, please, Famau Ali.

**Famau Ali:** Salaam Aleykum, niko na maelezo na maoni, kwanza nawakaribisha sana kutoka kwa safari ndefu sana huko mulipotoka mpaka mkafika Kiunga, sababu Kiunga ni mbali sana, ni mbali sasa hivi imekuwa mara mbili, sababu ni mbali kwa kaskazi ni mara moja peke yake, wakati wa kiangazi ni mara moja yaani wakati kusi inakuwa mara mbili sababu wajua safari ni nzito, kwa hivyo karibuni nimeshukuru sana kutuletea mwangaza kama huu.

Maelezo hayo, sasa mimi maoni yangu niku zungumza kulingamana kwa upande wa shule kulingamana klasi wani mpaka klasi ya nane na maoni yangu, iwe ni bure masomo, isiwe ni yatatiza ya kwanza.

Ya pili kuna masikitiko makubwa kulingamana na leseni za kuvulia, sababu leseni zakuvulia kuna leseni tatu tunalipa sisi, na mwenye duka ni moja peke yake. Kuna leseni yakuvua, kuna leseni ya madondo kuna leseni ya majongoo, tatu.

Sasa na upande mwingine kulingamana na mikoko sababu kama mimi ni masikini, baada yakuwa masikini mimi nimeenda kukata miti ya nyumba peke yake si ya biashara sasa kwa hivyo, kitu kama hiyo mimi ni maskini siwezi kutaka miti, kuangalia makuti, kuangalia mawe, kwa hivyo nataka vile mambo yalivo, kukata miti ya nyumba iwe sina malipo, sina payment, miti ya nyumba yangu, miti ya nyumba binafsi si ya biashara, wewe nisaidie ikiwa kama maskini mimi.

**Interjection:** **(inaudible).**

**Famau Ali:** Na ingine mimi nataka kuuliza tena yale maoni yaliotolewa mara ya kwanza iliandikwa au tujaribu tena, wajua ku ripiti.

**Com. Mosonik:** Hiyo mlikuwa mulitowa maoni siku gani?

**Mr. Famau:** Kuongezea au kufafanua zaidi?

**Com. Mosonik:** Unajua kwamba leo ni mara ya kwanza kukusanya maoni, pengine kulikuwa na wakalishi ya Tume wakifanya mafunzo Civic Education, lakini leo ni siku yakutoa maoni tafadhali endelea.

**Mr. Famau:** Mafunzo hatukupata, sasa hapa wajua maoni ya ghafla, walikuja watu mara kwanza kwa kutueleza kuwa mta elimishwa lakini ni kama mara ya kwanza sababu hi Katiba maoni watu ni kukaa mapema wakajiunda na maoni, hii ni ghafla leo, mtu ana maoni yakamtoka sababu binadamu anazungumza hi kesho ikamtoka, au alasiri ikamtoka kwa kichwa, hasa taimu kama hii, yakukaa watu mapema wakajianda kitu gani kina kuja wakajipanga, lakini ghafla ghafla wajua hata maoni yanapotea?

**Com. Mosonik:** Haya endelea.

**Mr. Famau:** Sasa kwa hivyo sisi hapa ni watu Kiunga Division, hii hasa Kiunga town hapa tuko mbali sana. Kwa hivyo maoni yangu, twataka tuwe kama mtu aliyeko Mombasa na hapa kuwe sawa. Wasikia bwana, kuna shida nyingi hapa Kiunga kuna matatizo mengi, maanake mimi niko na maoni kuna maelezo.

**Com. Mosonik:** Endelea.

**Mr. Famau:** Sasa waona kama hii, dawa wajua katika hospitali kuna matatizo, madakatari, sisi wajua hatuna, hata ukiwa

mgonjwa Kiunga mbali sampuli hii hakuna ndege, ya pasa wajua hapa Kiunga kuwe na gari, kuwe na boat mkokoni wakati wa kiangazi. Sababu wajua mtu hu ana nyakuliwa moja kwa moja anfikishwa kwa matibabu. Yaani hapa town pakingia hapa kipindu pindu watu wote wanaweza malizika. Nafikiri maoni yangu mimi hapo nimekomea nitawachia wenzangu wajua nafasi, sababu siwezi kusema yote, kuna wengine wana haki yao waseme.

**Programme Officer:** Kuja ujiandikishe.

**Com. Mosonik:** Hapa sasa ningependa kumuita Omar Ismail, *yeye ni observer*, sasa Osman Bamwati.

**Osman Bamwati:** Maoni yangu mimi ni kufuatana.

**Com. Mosonik:** Yeye ni observer, Mohamed Ngoma.

**Mohamed Ngoma:** Ma-officers mulokuja leo, kwa kuzidi kwazidi kutatulia wananchi mambo ambayo wanahitaji na kujua undani wao ma officers wa Katiba, kwa hivi leo tunashukuru sana, lakini maoni yangu ni kidogo kama swali lakini naendelea kidogo, ikiwa ni grupu ikiwa ni mimi mwenyewe kuhusu kwanza Katiba, kwa sababu tumeambiwa pale katika heading ya kile kitabu kekundu kule kwamba tunauliza swali,

**Com. Mosonik:** Kwanza sema jina lako.

**Mohamed Ngoma:** Jina naendelea bwana hakuna shida. Na tafadhalu kuna mambo kadha, naendelea na jina langu haita kosekana ita kuwa ndani. Kwa hivyo kwanza lazima niwachukuwe kwa sababu mumekuja ili (inaudible) mazungumzo ni marefu sana, na kina mama vile vile wote ma officers mulikuja hapa tuna shukuru lakini shida kubwa sana, sisi tunataka kujua kwanza Katiba ni nini?

### **Interjection Commotion**

**Mohamed Ngoma:** Haya basi nimekuwa kazi, Ma officers munakuja hapa wote kuhusu mambo ya Katiba. Kina mama na wavulana wote mlokuja hapa, Ma officers tunashukuru sana. Bw. Officer nitarudia pale pale uliokuwa umenitoa makosa kuhusu habari ya jina nitatangulia jina kabisa, mimi naitwa Mohamed Ahmed Ngoma, jina maarufu naitwa Ngoma. Nafikiri Ngoma hata mtoto mdogo ukisema Ngoma inakuja tayari kwa sababu ni drummers kwetu.

Kuhusu maswala yangu ni swala moja kwanza nauliza swala kuhusu Katiba, kwa sababu tumeishi Kenya hii kutoka sitini na tatu tumeona mambo yalikuwa yanaendelea kama kawaida kupatikana huru halafu imekuja mpaka kwa mzee Moi ambae tuko nayo tuliona mambo yameendelea kama kawaida kuja 92 tunaona mambo mengi yamevurujika, kwa hivyo sasa tunataka

kujuliza kitu Katiba ni nini? kwanza Bw. Ma officers halafu sasa tuendelee na mazungumzo hayo.

**Com. Mosonik:** Sasa nilikuwa ninafikiria kwamba sisi wote tumejua Katiba ni nini na tumekubaliana kama wa Kenya, kwamba tungependa kurekebisha Katiba. Katiba ni sheria kuu ya ki msingi ya nchi. Na umetaja ukweli kwamba mwaka wa sitini na tatu tukapata Uhuru tukawa na Katiba yetu. Wakati wa ukoloni sheria kuu yaki msingi ya nchi ilikuwa ni sheria ya ukoloni ya mfalme ama malkia wa uingereza. Tukapata Uhuru tukapata tukiwa na Katiba, ambayo ilitangazwa ama ilianza kufanya kazi tarehe kumi na mbili mwezi wa Desemba, mwaka wa sitini na tatu. Hiyo Katiba ndiyo imetawala mpaka wakati huu, ama tumeitumia kujitawala. Lakini tena tunajua ya kwamba hiyo Katiba ya mwaka wa sitini na tatu, imebadilishwa mara nyingi na pengine nyinyi mnajua katika area hii kwamba Katiba ya kwanza ya Kenya tulipopata Uhuru mnawenza kusema ilikuwa ni Katiba ya ki majimbo, ilikuwa na mambo mengi lakini kitu kimoja ilikuwa kuna utawala wa majimbo.

Kulikuwa na bunge yenyeye vyumba viwili, kulikuwa na viongozi wengine wanaitwa Senators pengine mnajua mambo mengi kama hayo. Lakini sheria hiyo kubwa kuu ya Kenya imepata kubadilishwa kwa hii miaka karibu arobaini tangu tujitawale karibu mara arobaini, karibu kila mwaka inabadilishwa lakini, inabadilishwa na wabunge bungeni bila kuwahuishwa wananchi.

Katiba ya kwanza ilijadiliwa London kati ya viongozi wa Kenya wa vyama vya siasa na serikali ya uingereza. Viongozi kutoka sehemu hii moja mnajua alikuwa ni Ronald Ngala, mwingine kama Matano na wengine, lakini wakakubaliana tukapata Uhuru Baada ya Uhuru sasa wabunge wetu wakiwa bungeni wamekuwa wakibalisha Katiba.

Hata mwaka wa tisaini na mbili, Katiba ilibadilishwa kwa ajili ya kifungu ya 2A ilikuwa inasema Kenya itakuwa ni nchi ya chama kimoja halafu ikabadilishwa, kulikuwa na mabadiliko mingi. Ndio mwishowe mwananchi, na Serikali wakakubaliana tuwape nafasi raia wenyewe wakati huu, wafanye marekebisheso, sasa raia wenyewe hawawezi kufanya marekebisheso bila kuwa na chombo fulani cha kutumia.

Chombo cha kwanza kikawa ni Tume yakurekebisha Katiba ndio sisi hapa, lakini chombo cha pili ni wananchi wenyewe, wakiwa sehemu yao ya uwakilishi bungeni, inaitwa Constitutency forum tukiwa tumeketi kama sasa hapa tukijadiliana maneno ya Katiba. Sisi ni chombo cha pili cha kurekebisha Katiba, sisi tukiwa wananchi wenyewe kwa sehemu zetu za uwakilishi bungeni.

Halafu baada ya hapo maoni haya yote kama nilipokuwa nimeeleza tutayapeleka kwa mkutano mkuu wa taifa, inayoitwa National Constitutional Conference. Sasa maoni hayo yote yatajadiliwa ndio tusikizane kuhusu Katiba mpya.

Chombo cha tatu, Mkutano mkuu wa taifa, lakini tukiwa kwa mkutano mkuu wa taifa na hakuna masikizano, hatusikizani kuhusu Katiba mpya kutakuwa na chombo cha nne cha kurekebisha Katiba hiyo ni kura ya maoni, tatarudisha swala kwenu tena, kusema pengine kulikuwa na mapendekezo kusema tunataka utawala wa Majimbo, lakini wengine wamekataa kwa mfano, ama kwamba kina mama wawe na uwakilishi bungeni sehemu kiasi fulani lakini hatuja sikizana kwa mkutano.

Tunarudisha swala kwenu mpige kura ya maoni, hicho ni chombo kingine cha yakurekebisha Katiba. Halafu baada ya hapo, haya yote yatapelekwa bungeni na wabunge wapitishe ndio kuwe na Katiba mpya.

Kwa hivyo Katiba kwa ufupi ni chanzo cha sheria kuu cha ki msingi, chanzo cha sheria zote ambazo hata yametajwa hapa, kwamba licence, kuna tax inasumbuwa watu kwa ajili gani walipie makuti ya nyumba na mambo mengi mengine, yanatokea yote ukichunguza kwa makini kutokana na sheria ku yakimsingi, yaani Katiba.

Wakati wa ukoloni kulikuwa na sheria zingine za wakoloni. Kama kule kwetu bara tunatoka sehemu ya ardhi kubwa ilikuwa imenyakuliwa na wazungu, kulingana na sheria kuu ya wakati ule, tukapata Uhuru wengine wa bara wakapata mashamba, lakini hiyo si kusema kila kitu kiko shwari.

Sasa hii fursa ni kwenu kusema maoni yenu, tukitaraji kwamba mlipata masomo na kama hamkupata masomo ni bahati mbaya lakini, ingawa hamkupata masomo, kwa waingereza wanasesma, “the wearer knows where the shoe pinches,” mtu ambae anavaa kiatu ata anasikia yeye mwenyewe bila kujua aliyetengeneza kiatu, hiyo kwamba kinamfinya, kwa hivyo zile problems zote mlizonazo muziseme tu, halafu tutafanya yawe maswala ya kiKatiba nimeeleza kidogo, sasa tafadhali.

**Mohamed Ngoma:** Asante sana Bw. Mwenyekiti wa Tume hii, angawa sikuui kwamba ni mwenyekiti lakini nakuona ndio mwenye kiti tayari, mwenyekiti wa Kamati hii ilokuja hapa, very good, kwa hivyo pia nakushukuru sana kwa maswali yangu nimekuuliza na umenijibu vizuri na nafikiri wananchi wenzangu mumefahamu vile nilivo uliza na kujibiwa?

Response from the crowd: sawa, bado, wengine bado wengine sawa, Tumefahamu. Okay

**Mohamed Ngoma:** Sasa Bwana Mwenyekiti, wakati wa hayati nafikiri mambo yalikuwa yanaenda kiswhari kwamba Katiba ilikuwa imeruhusu mwana nchi awe na kama haki yakumilki ardhi, hiyo Katiba, ni sababu ni mojawapo katika Katiba zile za zamani.

Mwananchi ni lazima awe na kibali ya kitambulisho kwamba ni mwananchi, na mtu ambae (inaudible) kwa njia lolote alikuwa na haki kwamba Kenya ina toa kama kawaida kibali ilikuwa inapatikana, lakini wakati huu wa sasa kila inapobadilishwa Katiba mambo yanazidi kuburujika.

Kwa hivyo maoni yangu naonelea kuhusu mambo ya uridhi, ni mambo ya dini. Mambo ya uandikishaji wa kazi kwa wanawake wa Kiislamu kwetu hairuhusu, ni ki maisha tu, hiyo Katiba haikusema hivyo. Katiba ya Kiislamu inakataa.

Hii haki yakumiliki ardhi mwananchi lazima apewe kwa hivyo lazima tuwalaumu viongozi wale wa Serikali wanao pewa zile nyadhifa ndio hawatutumikii sisi wananchi, pembe zote za Kenya. Kwa hivyo naona hakuna haja yakubadilishwa mawazo ya

kwamba ati tubadilishe Katiba, tufanyeni no, mambo yale nafikiri yalikuwa yanaenda ki shwari, isipokuwa tu yaliharibika kwa watumishi wenye kupewa zile nyadhifa. Kwa hivyo naona tutapoteza wakati watu wawe wakijenga Kenya hii sisi tukijadiliana mambo ambayo yatakuwa hayana msingi na watu nawatasonga mbele. Kwa hivyo hayo yangu machache nafikiri asante.

**Programme Officer:** Haya jiandikishe.

**Com. Mosonik:** Tueedelee please, Athmani mzee, hata yeye ni observer? Okay, na Hamza Bwana,

**Hamza Bwana:** Assalamu Aleykum. Mimi langu kusema

**Com. Mosonik:** Jina lako kwanza.

**Hamza Bwana:** Jina langu ni Hamza Bwana. Mimi langu kusema sisi hapa Kiunga tuwe na Uhuru kama wenzetu walikuwa nao. Shauri sisi hatuna Uhuru kamili, Uhuru wetu ni wa matatizo. Tena kama huko bara walikuwa wazungu, wakatolewa kisha wananchi wakapata sehemu walipo kalia. Sisi kupata Uhuru tulikuwa tuna bahari sasa wazungu kinajuli wana (inaudible) kisha hatuna pa kutoma, liseni watu wa tutome, hapa kumewekwa jiwe. Kitu kingine kama hapa makoko, hatuna ruhusa yakukata, nimeshindwa na mambo hayo, kwa mkoloni pia ilikuwa hakuna, ijapokuwa ni kutoa karatasi na unaenda unakata kuni yako unakuja kuitumia. Leo ukionekana tu huko askari tayari, si waona Uhuru wetu sio Uhuru ni matatizo, hauna mpango.

Kwa hapa tunataka Katiba itufuate kama wale watu ambae wana Uhuru tu, barani huko tuko wenyewe kama tuko la zamani, tutumie kwa liza, kwa kukata mbao, miti na mambo mengineo.

Kwa upande wa bahari tuwe na Uhuru kama zamani hakuna leseni wala hakuna chochote, mtu akiweza kuvua anateremka mwenyewe anakwenda zake baharini kuangalia mambo yake, si yo oo kuenda kaurini, ama mwanamke kushika madondo anashtakiwa, lete leseni, lazima utoe leseni, ikiwa hauna ni shida, kwa hivyo yangu mimi nakomea hapa, na sisi tuwe na huru kama waliopata Uhuru wengine basi.

**Com. Mosonik: Lali Kombo.**

**Mr. Lali Kombo:** Mimi jina langu ni Lali Kombo. Katika maoni yangu mimi nasema kwanza tukiwa Waislamu, huyu Khadhi wa Wilaya, District Khadhi ni lazima awe amehitim uelimu ya Kiislamu sawa sawa, uelimu ya dini sawa sawa, awe ni mtu ambaye ametoka University yoyote ya Kiislamu ambae imekubaliwa. Siyo kwamba tuna ma Khadhi sisi hata kusoma Quran hawajui, kuna ma Khadhi wetu ndungu zangu kwamba hawahisi kuisoma, lakini sasa kwa sababu yeye alisoma skuli. Kule skuli kuna somo la itwa I.R.E., somo la Kiislamu hati akapata yakwamba yeye ajua kizungu sana ndio sasa yeye amekuwa ni Khadhi. Na

alipokwenda kule alifanyiwa interview na watu wasiokuwa Waiislamu. Kwa hivyo sasa mimi naona maoni yangu ni kwamba hawa ma Khadhi wetu wote wa wilaya ni lazima wawe watu ambaye wamehitimu kutoka University yoyote ya Kiislamu.

Maoni yangu ya pili inasema ya kwamba, kama vile ambavyo imewekwa siku ya ijuma pili iwe ni sikuku kwa watu wote, kwa hivyo na siku ya Ijumaa pia iwe ni sikukuu hapa Kenya kwa watu wote, Waiislamu na wasiokuwa Waislamu, watu wote wasiende kazini, kwa sababu vile jumapili imewekwa pia ijumaa iwekwe, hiyo jumamosi ni shauri yao kama wataiweka ama wataindoa, lakini hii sikukuu ya Waislamu iwe ni sikukuu pia kama sikukuu ya jumapili.

Maoni yangu ya tatu nasema mtoto yoyote ikiwa mzazi wake moja ni Mkenya, kwa hivyo huyo mtoto pia awe Mkenya bila yakujali jinsia yeyote. Kama ilivyo sasa hii kwamba baba akiwa ni Mkenya ndio mtoto ni Mkenya. Ikiwa mama ni Mkenya baba si Mkenya ati mtoto si Mkenya. Kwa hivyo maoni yangu mimi naona isijali jinsia ikiwa mzazi yeyote ni Mkenya kwa hivyo mtoto naye awe ni Mkenya.

Maoni yangu ya nne ni kwamba hii bahari ndio shamba letu sisi, kwa hivyo utaona kwamba wakulima wakenda kulima kule hawatoi leseni, hawana leseni yeyote. Lakini sisi wavuvi tukienda pale tunaambiwa tutoe leseni kwa sababu gani? Kwa sababu watu wa hapa wote ni wakulima. Lakini sisi watu wa Pwani sisi twaonewa kwamba sisi ndio watu wa uvuvi, kwa hivyo tuwashike shike, kwa hivyo mimi naona maoni yangu ni kwamba, hizi habari za leseni zote ziondolewe kwa wavuvi wote. Ikiwa mtu anataka kuvua aende bure, wanawake kwenda tunga kauri wote wende bure, hakuna habari za leseni.

Maoni ya tano nasema kwamba ma Mayor wa City Council na wenye Viti wa County Council wachaguliwe moja kwa moja kutoka kwa wananchi, sio kwamba wale ma Councilor wamekwenda kule wanapewa pesa basi kila moja anajua la, ule Mayor mara nyingine sisi hatumtaki huyo utudulumu lakini kwa sababu vile ye ye amepata kule ameshika wale watu ndio mara moja ye ye ni Mayor, lakini sasa mimi naona kwa maoni yangu sisi tuwachague ma Mayor na Wenye Viti wa ma Baraza mmoja kwa mmoja wachaguliwe na wananchi.

Maoni yangu ya sita, na sema kwamba kumiliki ardhi iwe ni sisi wenyewe hapa, Kamati zile za wazee ziliokuwa hapa, ama baraza lile la wazee liliko hapa ndilo litowe ile stakabathi ya sisi kumiliki ardhi ili ijulikane kwamba fulani ardhi hii ni yake na anaweza kuimiliki. Sio kwamba watu wako Nairobi, ati umiliki Ardhi mtu ajua Ardhi ukienda huko Nairobi ukimjua mtu hata Kiunga aihiisii lakini atakuletea barua ya kwamba ardhi ya Shekani ni ya mtu fulani. Hiyo isiweko, maoni yangu minaona watu wapale pale kijijini ndio mwanzo watoe hiyo stakabadhi iende ipitiekama itapitia kwa Chifu, kwa Sub-Chifu kwa D.O. mpaka ifike huko ndio sasa ije karatasi yake yakumiliki ardhi, siyo kwamba mtu atoke na karatasi yake kutoka Nairobi, aseme mimi nimemiliki ardhi Yambo, amemiliki ardhi Kui, amemiliki ardhi Roko hiyo isiweko. Kwa haya maoni yangu sita nawashukuru.

**Com. Mosonik:** Asante sana, sasa tumsikize Bw. Heri Ali Sizi

**Mr. Heri Ali Sizi:** Assalam Aleykum Warahmatullahi T'aala Wabarakatu, kwa jina naitwa Bw. Heri Ali Sizi na mimi nafanya kazi ya ukulima. Kutetea yaani nataka kutoa maoni kibinafsi na kuchangia watu wote. Maoni yangu ni hivi ya kwanza, kwa upande wa ukulima, katika Kenya hii hapa nilipo Kiunga, ni kama niko na kitambulisho kimoja tu peke yake, na mpaka dakika hii sijajihisi kuwa ni mwana Kenya, maanake kitambulisho kile ni cha public peke yake.

Nina shamba pale chini lakini hata naiogopa kuweka mimea kulingamana sina karatasi, leo hii nimeweka mimea wangu, mara mtu ametoka na makaratasi yake Nairobi amesema hiyo ni ardhi yangu nita fanya nini? Kwa hivyo nataka Serikali ya Kenya injue kama mwana Kenya na inipatie haki yangu ya kumiliki ardhi. kwa sababu nimesemea kama miaka kumi hivi ya upandaji miti peke yake. Niko na ujuzi ya miaka kumi hiyo ni kama miaka kumi ya bure imepoteza nataka kupanda miti naogopa Serikali ya Kenya haini patii haki yangu. Ma Officer walioandikwa kazi wanaogopa Kiunga ni mbali, wako na pesa wengine, wanatoa pesa zao huko wanajiandikisha ma ardhi huko huko, mimi naletewa tu karatasi, Bwana hapa ni pangu. Sasa mim ni mwana Kenya? Naambiwa mimi niko huru, lakini inaonekana mimi sina Uhuru ye yeyote yakuishi hapa Kenya. Kitambulisho cha public peke yake hakinitoshi kuishi hapa Kiunga, mpaka nihakikishe nami nimepata ardhi yangu, la sivyo officer atoke huko aje hapa atugawanyie mashamba. Angalia sehemu zingine za bara ziko ma karatasi yake kwani wale ni wana Kenya, sisi si wana Kenya? Huku lazima Serikali ya Kenya wasikae tu chini huko wakasema basi tumepanga kitu fulani tu hivyo na kipitishwe bungeni, lazima kwanza waje kwetu tuko na wazee wa kijiji tumeandikiwa ma Chifu. Wapitie hiyo njia kwa wazee wa kijiji waende kwa ma Sub Chifu waende kwa Chifu halafu sasa ndio mambo iende juu. Lakini siyo mtu akae juu mezani afikirie kwamba Kiunga kuna ploti yangu, hata Kiunga hajui mahali iko. Yeye anasema Kiunga kuna ploti tu mimi ni yangu. Sasa mimi nina faida gani yakuishi hapa Kenya? Ama niko na faida gani kuambiwa mimi ni mwana Kenya eh, kwa hivyo maoni yangu ni hayo kidogo tu sina mengine.

**Com. Mosonik:** Omar Mujahid.

**Omar Mujahid:** Jina langu ni Omar Mujahid Omar Lali, maoni yangu ambao natoa ni kwamba tunataka tuwe huru kama tulivyo kuwa wakati wa Ukoloni, ambapo katika sehemu zetu za Coasti, uvuvi tulikuwa tukiwachia free tukiwa bahari yetu. Sisi watu wa Pwani hatuna pareto, hatuna kahawa, hatuna majani ya chai. Sisi lengo letu tumetegemea Bahari na ukulima wa mahindi kwa sababu hii ardhi yetu ni ukame kwa sababu mvua ni masiku mpaka masiku. Kwa hivyo twaomba ya kwamba wale wahusika mashirika kama yanakuja, kwa upande huu wetu wa Coasti yawe Serikali kwanza ichunguze na kupitia kwa wananchi ili kujua madhumuni yao ni nini, wataangamiza wananchi au watakuwa na manufaa ya wananchi.

Kwa hapa kwetu Kiunga ni sub-location ndogo tuna reserve nne sasa, ambapo hapa Pwani, hapa mwituni huwezi kufanya kazi yako kwa ukamilifu. Ukienda baharini huwezi kufanya kazi yako kwa ukamilifu kwa sababu sub-location moja ina reserve nne na maana ya reserve ndio tayari Park. Sasa leo sisi kama wananchi ambao tumekaa hapa maoni yetu tutatoa sisi wananchi ambao tuko hapa, ikiwa hapa walikuwa ni wanyama, wanyama hawatoi maoni, wanatoa maoni. Ni wananchi ni haki kwamba sisi wananchi tujulishwe kwa haya mashirika. Kwa sababu mashirika yanakuja hapa, ni mashirika yakuangamiza. Kama hili

shirika tunalo hapa la juzi ni shirika ambalo limeangamiza kabisa wananchi, hawana manufaa wala hawana jambo lolote wanadolipata.

Kwa sababu shirika sasa ni karibu miaka sita, hakuna mvuvi hata mmoja amefaidika kwa nyavu au amefaidika kwa boat, au amefaidika kwa machine au amefaidika kwa loan. Ni yetu tafanya mipango na kuishi hapa.

Kwa hivyo tunataka tuwe wakati wa Ukoloni na hayati mzee Kenyatta alipokuwa tukawa uvuvi tuna haki. Sasa mimi kama Captain au nina boat, boat leseni, nami uvuvi leseni na bibi yangu nyumbani leseni. Mimi mvuvi mmoja nina leseni nne, ya boat, yangu yakuvua samaki, nina ya madondo, nina ya kaure, nina ya mayongo.

Kisha mimi mvuvi natoka hapa saa kumi na mbili mpaka saa kumi na mbili, ikiwa shirika lataka kuhifadhi, sisi kutoka kale tumehifadhi, na mpaka sasa twahifadhi. Hatukatai mambo yakuhiadhi. Lakini sasa leo mimi nimeenda baharini kutoa nimepambana na kamba mwenye mayai, na leo kwangu watoto wangu ni kumi na nane na wake nilio nao ishirini leo hawana chakula, kwa hivyo Serikali irudishe mashika iwe kile kitu ambacho hakifai wa nunue watafute birika watie, siyo kwamba uvuvi nitatukua kwa sababu ni njaa, na nikiwa na njaa nita jepa nitakuwa mimi sina mipangilio.

Kwa hivyo tunataka kuhusu mambo ya Kasa yasitoke nje bila kushauriwa sisi. Tunataka katika mambo yote tushauriwe sisi. Sasa Kasa katika mkoa wa Pwani kwote kutoka Kiunga Shakani mpaka Dar-es-salaam mpaka Lunga Lunga Kasa huna ruhusa kula. Na sisi tukiinuka kwetu na wazazi wetu na mila yetu ya ki Bajuni Kasa kwetu ni dawa, kifua, homa, matumbo, baridi kila kitu. Lakini leo mashirika yamekuja (inaudible) hakuna Uhuru kwa wananchi. Uhuru umekuwa ni wa mashirika kwa hivyo tunaomba kuhusu mashirika,kwanza Serikali ikae nao chini ione kama itafaidi wananchi au haifidi wananchi?

Kama mambo ya makoko tumekosa kujenga, ukiona hizi nyumba zimekosa kujengeka kwa sababu makoko tunalinda sisi wenyele wananchi, kama ni Shirika halindi, sisi wenyele wananchi wa Kiunga ndio tunalinda. Sasa kuchinja makoko mpaka kuja nao hapa inagarimu mti ishirini ulipe shillingi mia sita, wewe ni maskini baharini unapata 20 shillings per day una kitu gani utapata. Kwa hivyo naona hii ni dhuluma, kwa hivyo tunataka kupita sharia yenyenye mipangilio ya kwamba kutoka jadi na kila jamii na kila kabilia ina mila yake ina dasturi yake.

Waislamu wanapitia kwa La Ilaha Ila Lahu na mtume wao Mohamadi na Wakristo wana sharia yao, wana mila yao. Kwa hivyo kila mtu afuate ile mila yake na desturi zetu ambazo tukonazo hapa. Kwa hivyo sasa wakati huu nyinyi Tume ya Katiba ambao mumekuja hapa, mkituangalia mtatuona sisi ni wanyonge sana. Sisi tunashukuru kwa sababu tumekuja kuangaliwa na Katiba hii twaipanga. lakini wakati wowote sisi tulikuwa tunaenda holela tu, tunaenda tu, tumekaa tu kama mnyama alivyo kaa mwituni nasi tume kaa hivyo hivyo na wenzetu Wa boni na wote.

Kwa hivyo nasi tunataka tuhudumiwe kama wananchi walioko Kenya, mtu wa Kisumu anavyo hudumiwa na mtu wa Kiunga

ahuudumiwe, mtu wa Nairobi anavyohudumiwa na sisi tuhudumiwe. Ma officer wakiwa hapa siyo kwamba tuwe na ma officer hapa Kiunga lakini ofisi yao ni Lamu, hapa Kiunga pia officer hakuna. Kama ukija Idara ya Ilimu utaadhirika aliyoko ni Walimu, matatizo ya Walimu hakuna mwenye kusuluhisha isipokuwa officer mkubwa huko Lamu. Ukija kwa hospitali utaadhirika na mkubwa wa hospitali hapa hakuna. Hivi leo kukaingia kipindu pindu tu utaadhirika ni yupi alioko ni mwenye kulinda tu hakuna mtu yejote kwa hivyo tunataka nasi tuangaliwe kama wananchi wa Kenya.

Vile mumekuja sehemu yetu ya ubunge kama vile (inaudible).....sisi tuwe na haki. Nakomea hapa yangu ni mafupi.

**Com. Mosonik:** Athman Bahero, observor hata yeye, na Kasmani Gumi, hata yeye ni observor - Yusuf Kitete Boni Community.

**Yusuf Kitete:** Assalam Aleykum, Mimi naitwa Yusuf Abala Morsa lakini najulikana ni Kitete. Mimi natoa maoni kadha kuhusu Waboni na kuhusu Division hii ya Kiunga. Division hii ya Kiunga ina location mbili, Kiunga location na Basuba Location. Katika hii Division sisi tumeonewa na mashirika, mashirika wakati huu ni manne, kuna WWF, kuna KWS, kuna Dodori National Reserve, Boni Forest Reserve. Sasa haya mashirika manne yako Division hii. Na Lamu District kuna division nyingi, zote hazina mashirika ni hii tu imenyanyaswa na hawa shirika, ukienda baharini huna nafasi, ukienda huko barani kulima huna nafasi hapa ni ya Dodori Reserve, hapa ni Boni Forest, hapa ni Lungi Society forest hata hatuna mahali pakukanyaaga.

Pili sisi kabilia la Waboni ni kidogo katika Kenya, ningependa Katiba ituangalie nasi tuweke orodha kama wenzetu wa Kenya. Hii kabilia la Waboni inapatikana Lamu District Kiunga division. Sisi tunawenzetu, wakati wa shifta tumepoteana sasa wamerudi wako na sisi zaidi ya miaka kumi na mbili. Sasa ikiwa Chief anahakikisha ya kwamba hawa ni wenzetu, Chief hafai eti amechukuwa hongo, ikiwa headmen anasimama huyu ni ndugu yetu hafai, wazee wakitoa ushahidi hawa ni ndugu zetu wamekimbia wakati wa shifta wame rudi, wanatiwa ndani. Nani atatoa ushahidi na kuhakikisha hawa wenzetu ni ndugu zetu? Katiba ihakikishe wao ni wenzetu, na ni wana Kenya wamerudi kwao walienda makazi, walitorokea huko na sasa mahali walikuwa wakifanya kazi kumetokea shida. Wamerudi wanaishi na sisi kwa hivyo wapatiwe haki kama sisi. Awe ni Mbajuni, awe Mboni , awe ni Msomali, ni wenzetu wamekuja sisi hatuwezi kuwachukuwa kama maadui, ni wenzetu. Wapewe haki kama sisi.

Lingine ni kwamba Waboni hivi sasa ni maskini, lakini ni wanadamu kama WanaKenya wengine Shule hatuna, madaktari hatuna, hivi wakati wa campaign ndio Serikali inaanika corner fulani hakuna kitu, kuna fulani hakuna kitu, munaambiwa imekamilishwa, siasa zikiisha tunawachwa mambo yana lala, hiyo si haki

tupatiwe haki kama Wanakenya wenzetu. Shule iwe ya daima, hospitali ile dispensary tuliyo nayo iwe ya daima tupate matibabu na sisi ni wananchi a Kenya tuko, pembe ya Kenya, tujulikane hili kabile la Waboni ni kidogo nao waangaliwe wachangiwe waweko. Katika Kenya sisi ukisoma huwezi ona Mboni. Nilienda Nairobi nikasema mimi ni Mboni nikaambiwa kabile gani hiyu? , Sasa nashangaa nitatoa historia wapi, nataka sisi tujulikane, historia yetu ipatikane.

Serikali iandiikishe Waboni wako kama elfu nne. Waboni kuanzia hapa mpaka upande huo ni wengi lakini sasa umetengwa hatujulikani ni kabile gani, hatuna historia, hasa katika Kenya ukisoma historia iko kabile arobaini na mbili yetu haionekani imetoka wapi, ni Ormaba, ni Somali inaambatishwa mahali Boni Sanye, Boni Orma tuna taka nasi (inaudible) tuwe wana

Kenya.. Na siyo Serikali iangalie darubini yake wakati wa siasa, tuangaliwe shule, tuangaliwe ili ikisha imeisha tuangaliwe kama wenzetu.

Lingine Division hii, haya mashirika yamekuja kutunyanyasa tungependelea tukae pamoja na tuelewane, hatutaki masikizano yale ya mbeleni, maana wametunyanyasa, tusikizane ikiwa wataendelea ama tutawasimamisha. Sisi wenye we tuko ujingani hatuja erezuka, mpaka tuerevuke waje watufundishe sio kuja ee hii siku mbili inaadikwa hivi kisha wakaenda. Mweneye kujenga nyumba hapati miti Waboni wakitaka kupasua mbaa wafanye mlango hawapati kutatua tatizo kama hilo. Haya mashirika warudi kwa wananchi wapate maoni ya wananchi ndio wapate kuendelea siyo wapate kupata maoni ya Serikali ama ma officer wengine yakujisaidia wao wenye we na sisi huku tunaumia.

Lingine, hizi kazi za Serikali, ma department ambaa yananaajiri wakija kwa district wana gawanya kwa ma division, ikija hapa kwetu inatakikana form 4, sijui C+, sijui D-, sisi hatuna elimu upande huu hatujasoma, kunaletwa mwingine, anapatiwa hiyo kazi anaambibiwa huyu ni Mboni kumbe ni khabila lingine anaambatishwa kama Mboni, huyu Mbajuni basi anakuja mwingine hana ujuzi wa bahari anawekwa anazama kama nanga, na wenye we tuko sisi hatukusoma sisi. Twataka Katiba itupati haki yetu hata kama hatukusoma paka tutakapo fika tutakapoona mbele na sisi. Lakini isisemekane hawakusoma anaandikwa officer mwingine kutoka Kericho, Kirinyaga hatutaki. Hata kipofu anapelekwa, sasa hata bubu yuko na officer wake hapa na sisi tupelekwe kama bubu. Mpaka tupate kwendelea. Tutasomesha nini hawa watoto, ikiwa sisi hatukusoma. Hakuna form 4 hapa, tuandikwe tu kazi, tupate kazi hawa watoto wengine wapate kusoma. Ikiongojewa form 4 tuta amka lini sisi? na sisi tumetupwa pembe ya Kenya. Tupatiwe haki zetu, Mwalimu tupewe, Agriculture Officer tupewe, Forest Officer tupewe. Division hii ile haki yake ni watoto kumi wakigawanyiwa Lamu District, Mbajuni apewe nafasi tano na Mboni apewe nafasi tano. Tusiulizwe kwamba kama hatuna form 4 tuandikiwe vijana wengine kutoka huko na kuita huyu ni Mbajuni na huyu ni Mboni hatutaki hizo ni siasa tuangaliliwe kisheria na sisi tuwe sawa na wenzetu.

Mimi maoni yangu ya mwisho, khabila yote iko kwa studio Boni hakuna, nataka lugha yetu kidogo iwe kwa studio hata kama dakika tano.

Inginge sisi hatuna nafasi, Katiba iangalie haya maoni tunayoyatoa wananchi wa hapa, isiwe maoni yatawekwa pembeni haya maoni yetu yatolewe nasi tupate kusikika, hata kama mengine yata puuzwa mengine tuwe tunapata. Kwa hivyo sisi tumesahauliwa sana. Katiba safari hii ituangalie. Mimi nimetoa maoni yangu, nimefika hapo, naitwa Yusuf Kitete Abala nimekomea hapo nikiwa Basuba location Kiunga division.

## **Clapping**

**Com. Mosonik:** Yusuf Ali, observer hata yeye, okay, Abdulrahman Sheriff.

**Abdulrahman Sheriff:** Asalaam Aleykum, kwa jina naitwa Abdulrahman Sheriff. Maoni yangu ya kwanza ni kuhusu citizenship, uraiya. Kulingana na Katiba ya Kenya kuna njia kama nne hivi yakupata uraia. Ya kwanza ni kwamba umezaliwa Kenya, ama mzazi wako ni Mwanakenya, ya pili ni registration kwa uandikishaji lakini katika hii uandikishaji inasemekana kwamba ikiwa mwanamume ameoa mke wa kutoka nje huyo bibi yake anafaa kupewa urai lakini, mpaka afanye application na apeleke hiyo application yake kwa Minister. Kulingana na maoni yangu naona kwamba hiyo ni process ndefu na wengi wetu hawataweza kuyaandika namna hiyo, na nataka yaani ipitie direct kwa vetting Committee ambayo kama ya kawaida wanajua zaidi kwamba huyu kweli ni bibi yake na wameowana na hiyo ipitie kama njia ingine.

Maoni ya pili ni kwamba land ownership, yaani umilikaji wa ardhi. Katika umilikaji wa ardhi, ardhi zote ni za Serikali, yaani zina milikiwa na County Council. Lakini hii County Council ni watu ambao ni ma Councilors watu wadogo, kwa hivyo mtu yeoyote ama Serikali kama ni shirika ama ni watu binafsi wakitaka kuja kufanya kitu katika hiyo ardhi inakuwa rahisi kuwapitia wale watu ambaye ni wadogo, hata kama ni kuhonga itakuwa ni watu wadogo wanaweza kuhongwa. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba umilikaji wa ardhi irudishwe kwa public kwa watu wenyewe binafsi ambao wanaishi pale, ikiwa Serikali pia mfano yataka kujenga office, basi ipitishie kwa Committee ya watu waandikishaji wa ardhi. Committee ya ardhi ambayo iko pale kwa watu siyo ifanye kwa County Council.

Maoni yangu ya mwisho ni kuhusu election ya Local Government. Kulingana na sheria wanataka mtu awe amefikisha maximum of form 4, kama wenzetu hawa Waboni wamesema hawajasoma popote wacha kuwa na form 4 hata class 8 hawana, kwa hivyo nao pia wanatakikana wawe represented kwa Council, wasiwekewe kwamba ati ni lazima awe form 4. Tukisema kwamba lazima awe form 4 Mboni atatoka wapi? Mpaka hapo Asanteni.

**Com. Mosonik:** Ahmad Kuchi.

**Ahmad Kuchi:** Assalam Aleykum, kwa jina naitwa Ahmed Kuchi, mimi yangu nina mengi sana nilikuwa nataka wakati wa kutosha sijui kama ntaupata au namna gani?

**Com. Mosonik:** Dakika kumi.

**Ahmad Kuchi:** Kuna watu wanasherehekea uhuru wao kwa kujua siku mwaka ama mwezi. Sisi twajua uhuru wetu Tumepata 63 uhuru wa Kenya si wetu sisi watu wa Kiunga. Sisi uhuru huo hatukupata, 63 ndipo Serikali ilianza kuvunja majumba yetu kwa grader hapa, badala watu kujengewa Serikali hii yetu ndipo ilianza kuvunja majumba, kwa grader ili ati maadui wasijifiche. Kutoka siku hiyo mpaka hivi sasa, Serikali haijafikiria kwamba watu walivunjiwa majumba na sisi ndio tulizivunja hizo nyumba, kwa hivyo tuwape angalau ridhaa, hakuna. Kwa hivyo sitaki kusema mengi sana ingawa nina mengi.

Nataka kuelezea juu ya uhuru, uhuru tutakao sisi ni ule wa U-colony ambapo sisi hapa watu wa Kiunga, japokuwa kidogo

lakini watu wa Kiunga karibu kumi na tano, alikuwa kila mtu na gari yake. Sasa leo Kiunga hii ni mkokoteni mmoja tu, huu munaona ndio imemilikiwa ni watu wa Kiunga, basi.

Kisha upande wa suspect ya polisi. Suspect ya polisi inatumiza Bw. Mheshimiwa kwamba, pengine hapa katika hili kundi tulioko hapa, kukipatikana sigara moja ya bangi, badala ya polisi akishakiona kile kitu akiondoe akakitupe, watachukuliwa watu wote wakateswe kwa hivyo hiyo si haki. Polisi amekiona kile ni kibaya kimetokea kwenye watu haina haja watu gari nzima ama boat nzima kuteswa kile kitu kiondolewe kitupwe.

Jambo lengine twataka hukumu ndogo kama mfano wizi wa kuku, wa yai, wa kiberiti yasifkishwe kortini mambo kama hayo. Tuna wazee hapa, wanaweza kutuhukumia, kuna ma Chief hata kama ni adhabu watupe wao siyo kwamba sisi mtu aibe kibiriti apelekwe kortini. Ile kupelekwa tu kwanza ni mateso. Kwa hivyo jambo kama hilo twataka liondolewe.

Jambo jingine tunalotaka sisi ni kujua kwamba katika nyinyi mliokuja, katika nyinyi Kamishna wa Katiba watu wa kwetu hapa ni wangapi? Hilo ni swali kabla kuendelea nataka kuuliza kwa sababu tungelewana nao vizuri sana angalau kama hatukupata mtu wa kutoka hapa Kiunga awe ni wa Lamu. Kwa hivyo leo mtu wakutoka Lamu asimame tumjue ni huyu, basi ndio tuendelee na mazungumzo.

**Com: Dr. Mosonik:** Nilieleza kwamba Tume yakurekebisha Katiba ina Makashina ishirini na tisa, na kati ya hao wawili hawafanyi kazi full time wanaitwa ex-official. Moja ni mkuu wa sheria Mhe. Amos Wako na mwingine ni Katibu wa Tume anaitwa Mr. Lumumba, kwa hivyo tuhesabu watu ishirini na saba. Nilisema kwamba tukiwa hapa wenzetu wako, nilisema namna gani wako Mwatate, wengine Taveta, Matuga, Changamwe, Garsen, Magarini na Bahari. Sasa tuko watu ishirini na saba na kulingana

na sheria kila Mkoa ilikuwa lazima iweze kuteua kati ya watu wanne na sio chini ya watu wawili sasa mkoaa wa Pwani ina Makashina moja ni Prof. Ahmed Idha Salim pengine munamjua, alikuwa mwalimu wa historia,na alikuwa balozi, mwingine anaitwa Dr. Mohamed Swazuri, anatoka wapi? Kwale ama wapi? Kwale halafu mwingine ni Zein Abubakar kwao ni Mombasa na mwingine ni Abida Ali Aroni mwanamke mmoja wa Kiislamu ambae yuko na sisi, ambae ametoka Mombasa kwa hivyo Pwani wako watu lakini kukusanya maoni tunachanganyika, sasa tuko sote Pwani na hawakuja hapa lakini wako, wa Pwani sio wa Kiunga.

Ahmed Kuchi: Jambo la mwisho, twasikitika kuwambia twaunda Katiba mpya katika walopita na sasa ambao sisi tuko ya zamani hatujui, kwa hivyo twataka kwanza mutuambie ya zamani ilikuwa ni kadha kadha mpaka tuelewe, sasa tujue pengine munataka kuondosha jambo ambalo liko, na kwangu ni nzuri kwa hivyo twataka mutufundishe ile ya zamani kwanza, kisha tutoe maoni tuone ile ya zamani ilikuwa ni gani na gani. Kwa sababu mafundisho ni mafunzo hayo. Kwa hivyo twataka muwalete watu, wakutuelezea ile Katiba ya zamani, kisha watuambie sasa toeni mawazo yenu. Kwa sababu sisi hatujui Katiba za zamani zilizopita ni zippi za ukoloni nazetu wenyewe kwa hivyo kwa hayo nashukuru.

**Com. Mosonik:** Asante sitaki kurudia lakini tulisema leo na jana, ni siku za kusanya maoni ya raia Lamu ya Mashariki, kukusanya maoni tukiwa tunatarajia ya kwamba mumepata mafunzo, na mnajua Katiba ilisema namna gani. Lakini watu wengi wanasema hata hiyo Katiba kwanza haitapikani kwa ajili inauzwa kwa duka moja Nairobi inaitwa Government printers, na tena imeandikwa tu na kiingereza na kiingereza ile ya mawakili ya lawyers hata kuelewa ni ngumu. Ndio nimesema hata kama hamjasoma, si shida kwa ajili kitu cha muhimu ni kusema munashida gani, kwa ajili mkitafuta kwa makini mutapata kwamba shida zote zinaanzia kwa hiyo Katiba hata ingawa hamjui inasema namna nini. Kama hayo maneno ya ardhi inasema hamuwezi ridhi ardhi area hii kwa nini kwa ajili ya Katiba. Kwa hivyo sema yale unayajua, lakini maoni kukusanya ni leo kama hamkupata masomo yakutosha ni bahati mbaya, tumelewana. Sasa tumsikize Atik Atik.

**Atik Mohamed Atik:** Kwa majina naitwa Atik Mohamed Atik, nyumbani ni hapa isipokuwa kazi sasa niko Lamu. Commissioners, kwanza ni masikitiko makubwa sana, kwa sababu inaonekana kwamba watu wetu hapa hawakupata Civic Education. Nafikiri kutokana na sababu ambazo pengine Tumezielewa sisi ambao tuko pale, tukishauriana na Bw. Coordinator, lakini nitajaribu kueleza yale mapendekezo ambayo nitakuwa nikizungumza as an individual, na pengine kusaidia hawa watu wangu.

Pendekezo langu la kwanza Mabwana Commissioners utaona kwamba elimu ina shida ina problem fulani kwa hivyo ningonelea tuwe na elimu ya msingi that is basic education iwe ni bure na ni lazima ili kwamba mtoto apate elimu ya msingi atapo maliza primary level akaenda Secondary level basi pale ndio mahitaji ya fees yaingie kwa mzazi na hapa lazima kuwe kumeundwa zile Bursary Committees ambazo zitakuwa organized na ma Chief na wale local MPs. Kwa hivyo pendekezo lote ni kwamba hii elimu tunazungumzia nafikiri juzi kulikuwa na a lot of confusion, nasikia mzee anasema elimu ni bure lakini primary haziwezi kupeleka elimu kuna chalk kunataka kununuliwa kwa hivyo ikiwa ni bure irudi ile system ya zamani tulikuwa naye Kenya School Equipment Scheme KSES zirudi hizo, ili zisaidie hawa watoto. Ndipo hawa watoto kusoma hasa kwetu hapa watoto wengine wameshindwa kusoma kwa sababu yakuendelea na masomo yao.

Nafikiri mambo ya land ownership imezungumziwa sina haja yakuirudia. Nikienda kwa mambo ya matibabu Mabwana Commissioners, ni kwamba hali mnaiona nyinyi wenyewe, munaona kwamba sisi hapa tunashida. Hawa watu wana taabu za ki uchumi. Hospitali tunayo hapa ni Kiunga Health Center lakini utaona kwamba mzazi au mtu atakufa nyumbani, na pengine matibabu anaweza kuipata hospitalini, lakini hawezi kwenda hospitali kwa sababu ya pesa. Lazima watu walipe although tunaambiwa kwamba kuna hii mipango ya kwamba Committees zimeundwa kwamba zile pesa zitarudi hapa hapa hospitalini, kuendeleza hii hospitali. Hii ni kwamba Serikali imeshindwa kutuhudumia, zile basic rights ambazo sisi tunataka tupate kama wananchi, ni kwamba lazima sasa tununue yale madawa yakututibu sisi wenyewe. Ndipo pale waona watu wakikausha mikilifi wakinywa, wengine utasikia ni siba kumbe ni septic ulcer, na unasikia watu wana kufa tu namna hiyo.

Upande wa citizenship ma Bw. Commissioners, pendekezo langu ni kwamba kwa mfano, kama hapa Kiunga hivi sasa, tuna watu wetu ambao walikuwa ni wa hapa lakini kikazi walikuwa upande wa Somalia. Wamekaa kimaisha huko kwa sababu ya

matatizo ya Serikali wamehamia wamerudi hapa. Kwa hivyo inataka ichunguzwe kwamba mtu akisha fika miaka kumi, baraza la wazee limepitisha huyu ana haki kupewa awe ni citizenship, basi iwe hakuna mambo yakusukumana kwa sababu hapa kuna kamati zimeuundwa. Baadhi ya wazee hapa wamesukumana kutafuta kitambulisho mpaka sasa imekuwa ni ngumu, kwa sababu Chief hawezi kuweka kidole. Pengine anaweza weka kidole upande wa special branch itaonekana pengine mambo ingine mabaya. Kwa hivyo citizenship mtu hata akifika miaka kumi, iwe ni automatic citizenship. Ikiwa ameonekana kwamba yeze ana asili ya hapa Kenya. Sisemi Kiunga hata border zingine zote upande wa Ethiopia, North Eastern Province iwe namna hiyo.

Mambo ya security Bw. Commisioner ni kwamba, tunashukuru lakini hapa tuko karibu na mpaka, tuna Kenya Navy iko karibu na sisi, tuna Kenya Police ambao wako sawa wanafanya kazi mzuri lakini, mnavyo elewa kulingana na Department of Defence, rule ya kwanza inasema kwamba jeshi kama Kenya Army lazima liwe 100 miles from the border. Kwa hivyo hii ifutwe iwe instead of 100 miles waje karibu na zile border ambazo pengine zinatarajia wakati wote zavezakuwa na matatizo.

1992 nafikiri ikiwa sikukosea, kulikuwa na wakati wa Morgan, Bw. Commissioners baada ya kazi pengine twaweza kuwatemebeza tukawaonyesha pale tulipokimbilia, tulipandishwa kiwani huko, I was one of them karibu ku-drown, watu wengi waliumia wanawake wengine wakapigwa marisasi. Kwa hivyo tunaongojea Kenya Army itoke Baragoni ije isave wananchi katika hizi calamity, ambao zinatokea hapa. Kwa hivyo twaomba security iwe reinforced sisemi kwamba hawa hawapo hawafanyi kazi no, enforcement of security ile borders iwe ni sheria mambo ya 100 miles hakuna ifutwe.

Katiba mpya iseme kwamba security kila pahali, iwekwe katika border within the border kulinda mipaka ya nchi yetu.

Mabwana Commissioners, tumechagua wabunge sisi hapa, hivi unapoona hapa uko katika Lamu East kama vile unavyo elewa na tuna na m-mbunge ambaye sisi anatuwakilisha. Lakini hali hizi dhaifu mbali na kwamba pengine twakaliwa ngumu na Serikali lakini, pia, watetezi wetu bado hawajawa imara. Huu ni wakati ambapo yeze pia ningeomba angekuwa yuko hapa kuwajaribu kueleza pengine yeze ni mjuzi zaidi, amesoma mambo mengi zaidi, anajua Katiba, kwa sababu yeze ndiye mwenye kurekebisha hiyo Katiba, lakini ni bahati mbaya yeze hatuko naye hapa.

Kwa hivyo pendekezo langu kama Atik, ni kwamba wabunge wawe na routine visit kwa kila Constituency yake, na kila sehemu yake. Kisha kuwe na monthly report kila mwezi aweze peleka report na hiyo report atakayo ipeleka iwe signed by locational Chief ama baraza la wazee liundwe katika (inaudible). Kwa mfano katika workplan yake awe atakuja Kiunga kati kati ya mwezi, kisha hapa tuwe na baraza la wazee li sign kwamba huyu alikuweko hapa tumezungumza mapendekezo kadha, lipelekwa kwa katibu ya Parliament, ionekane kwamba huyu anafanya kazi.

Si kwamba yeze atakaa Nairobi watu wanaumia wanahangaika kisha kule anasema Kiunga hakuna shida, Kiunga sawa hakuna problem. Kwa hivyo, ikiwa kwa mfano MP ata-fail kufanya hivyo basi watu wawe na vote of no confidence, haraka election ifanywe si lazima kuwe na by-election mtu awe amekufa au vipi, hivyo kama mtu ambae amekufa.

Commissioners political, parties sasa nafikiri si kama sikukosea tuna arobaini na kitu ambazo zimekuwa registered. Naona ni madamu tumetoa kile kifungu cha 2A basi, mambo mengi yameanza kidogo kuharibika. Mimi naona, instead of hizi political parties kuwa nyingi sana, tuwe na tatu peke yake ikiwa ni lazima, lakini tukiwa na political parties mbili ni bora, kwa sababu moja itakuwa ni kama watchdog ya ile nyingine, sikuwa na NDP Kanu, sijui nini mara zinakuja kuungana mara zina kataa. Kwa hivyo political parties tuwe na mbili peke yake moja ikifanya kazi ingine ni watch dog yake. Kwa hivyo mtu atakuwa na Uhuru either ataingia kwa Kanu kuwe itakuwa political party

mwagine ataingia

political party ingine kama ni NDP, lakini iwe ni mbili tu. Kuwe hakuna mambo ya political parties kila kabilia iwe na political party yake. Political parties ambazo tunazo hapa Kenya ni za ki kabilia.

Mabwana Commissioners jambo la ardhi ambalo mimi nimesema limezungumzwa sana ni jambo la kusikitisha, lakini pia naona nigosie kidogo. Hapa kumepita Tume yakuchunguza wakati wa Njonjo Commission, wakaja tukajaribu kupatengeza nafikiri mpaka twaunda tena Serikali nyingine kesho kutwa ah mpaka sasa hakuna hiyo land ownership. Kwa hivyo ndio utaona hata vijumba vikianguka mtu hajengi kwa sababu ardhi si yake. Kama hiki chumba changu hapa sijengi kwa sababu si yangu. Kwa hivyo tuwe na board zile, villages board za kuongoza hii land management board. Ziundwe na zisikizwe. DC hana uwezo wa kusema kwamba huyu apewe ardhi huyu asipewe ardhi. DC ni mtu ni mfanyi kazi wa Serikali leo yuko hapa Lamu, kesho kutwa tunasikia ameenda Kapenguria.

Nafkiri Bw. Commissioner napenda kuzungumzia haki za akina mama . Haki za kina mama tunaona kidogo tumezigandamiza. Katika dini kama alivyosema mwenzangu ni kwamba pengine tuna limitations za kina mama, lakini lazima waangaliwe haki zao za ki sawa sawa. Nitazungumza ya haki za kwamba kuolewa na kuwacha iwe katika Kadhi. Constitution iwe kwamba ikiwa baba atatupa mama, divorce case imetokea, baba achukuwe jukumu a sign documents ahakikishe kwamba watoto atawsomesha mpaka wamalize masomo yao, na kila mahitaji yao awapatie. Si kwamba utaacha mke umetupa watoto kwa mama, ndio story imeenda umeenda kuo pahali pengine. Hawa mpaka wasaidiwe ndio nao watasadika. Nafikiri sasa hivi tuna child's right ambao nafikiri imepitishwa or unless it is in the process. Watoto haki za watoto kwa hivyo hiyo itiliwe mkazo Bw. Commissioners ya kwamba wakina mama wakiachwa basi watoto waangaliwe na mababa zao. Ikiwa mtu hata chukua jukumu hilo achukuliwe, hatua ya kisheria kama ku-commit suicide kwa watoto, ni kuwaua kuharibu maisha yao.

Kwa haya Bw. Commissioners nawapatia pongezi kwa kufika Asante.

**Com. Mosonik:** Asante sasa tumsikize Mwana Amina Shebwana Kiunga Women.

**Mwana Amina Shebwana:** Assalam Aleykum, Jina langu ni Mwana Amina Shebwana Committee Member wa Katiba, Lamu East. Maoni yangu ni kwamba tunataka Serikali itusaidie wakati wowote, ikiwa ni mchana ikiwa ni usiku. Ikiwa umeingiliwa na majambazi, ikiwa ni shifta umeenda kupiga ripoti polisi, tunataka watusaidie ifuatiwe hiyo ripoti wakati huo huo, siyo ikaliwe mpaka usubuhi, ndio askari waanze kuja nyumbani, hiyo ya kwanza.

Ya pili ni kwamba tunashida ya madaktari, madaktari wameondoka wote, ule ugonjwa ambae utatokea hautajulikana kwa hivyo tunataka ikiwa ni likizo daktari awe ni mmoja aende mmoja mpaka mwengine arudi. Sina mengine isipokuwa ni hayo.

**Speaker:** Mwana Umi Haji unamapendelekezo, maoni?

**Mwana Umi Haji:** AssalamuAleykum, mimi sina maoni

**Com. Mosonik:** Mohamed Kombo? Athman Lali

**Athman Lali:** Assalam Aleykum. Kwa jina ni Athman Lali, mimi niko na maoni kidogo sana, kwa sababu mengi yangu imeshasemwa lakini, maoni yangu ya kwanza kuhusu mambo ya hii cess ya County Council. Ingekuwa vizuri ile cess kusanywa na ma cess collectors wao kama hii Council yetu ya Lamu, pesa zibakie kwa zile zile division zake si zichukuliwe pesa hapa kama hapa kwetu huwa tukitoa pesa nyingi mwisho wamwezi inapelekwa Lamu hapa hata kichinjio hawawezi kutengenezea hata kisima cha maji hawawezi kufanya. Kwa hivyo pesa zile zile zitakuwa ziki baki hapa hapa ziungwe kamati hapa pesa zile zibaki kwa zile division naona itakuwa ni vizuri sana. Kwa sababu pesa zile zitatusaidia sisi wenyewe kuliko kwenda kusaidia watu wengine Lamu.

Halafu kuna hawa wabunge, na ma Councilors pia, ingekuwa vizuri muda wa miaka mitano ni mwengine sana, ingekuwa vizuri ikawa itapunguzwa ule muda kwa sababu ukichagua mbunge hapa ama Councilor akisha kupata hiyo kiti yeye kazi yake ni kunyakua pesa tu hataki tena kujua. Pengine mbunge utamuona mara mbili katika miaka mitano na pengine kumuona kwako ni kumuona yuwapita, hata kumwambia neno huwezi. Kwa hivyo uzuri wa mambo ibakie kama miaka miwili tu imetosha. Ikimalizika miaka miwili uchaguzi mwengine uanze, kwa sababu wengine hawafanyi kazi wakishapata ubunge basi wao ni kukaa tu. Wanakula raha na pesa zao kwa hivyo muda wa miaka mitano kwa wabunge na ma Councilors ni mwengine. Kuna wengine wanafanya tu ni kama biashara vile wakisha kupata wanakaa tu na kuchukua pesa.

Halafu pia kuna la mwisho, kuna hii dini ya Kiislamu, haitawezekana kama vile inavyo pangwa sasa, ati mwanamke awe na haki kamili kama mwanamume. Hiyo inatuingilia, kwa hivyo Katiba ile yakusemekana kwamba mwanamke awe na haki sawa na mwanamume hiyo itakuwa imetupeleka vibaya na kidini. Kwa hivyo iwe Katiba itatupatie Uhuru pia wa dini zetu, isituilingilie

hapo kwa sababu mwanamke ikiwa atakuwa sawa sawa na mwanamume, mwanamke anaweza kuja nyumbani badala ya wewe kumuambia, wewe umefanya vibaya yeze pia akuambie hata wewe umefanya vibaya. Wewe waingia kwa mlango huu na yeze kwa mlango ule, kila mmoja yuko na right yake kwa hivyo, hiyo itakuwa inaleta shida. Na mwanamke siku zote lazima awe chini ya mume, lakini ikiwa atapewa haki awe ni sawa na wewe, hiyo itatuletea shida kwa dini. Hayo ndio yangu kama nitakumbuka mengine nitakuja tena.

**Com. Mosonik:** Mwalimu Tajiri.

**Maalim Tajiri:** Asalaam Aleykum. Jina langu ni Maalim Tajiri, na maoni yangu ni kwamba, nataka sasa Tume hii ya Katiba ijue, mpaka sasa si hatuko Kenya. Kwa hivyo hatubadilishi Katiba. Ni kuunda Katiba, maana yake shauri Katiba iliyokuweko hatukuijua ilikuwa ya namna gani wala ni sampli gani.

Kuhusu mambo ya ulinzi, kidogo yaligusiwa hapa, kwamba jeshi huku Barigoni, ikitokea chakutokea huku ndio watu humalizika.

Kuhusu ardhi, mpaka sasa Kenya kupata Uhuru ni mwaka ngapi? Hakuna mwenye umiliki, hata nyumba yake ile anayeishi. Ile nyumba ushipo huna milki kwamba ni ardhi yako, je unayo moyo wakujenga hiyo nyumba?

Kuhusu mambo ya bahari ambayo, sisi huku hatuna mashamba, shamba letu ni bahari, utakuta kwamba mtu moja huambiwa akate leseni tatu. Leseni ya madondo na kaure leseni ya uvuvi, na leseni ya mayongo, ndio uende baharini. Je hiyo Katiba ya zamani ilikuwa (inaudible) nasi tuko Kenya? Kwanza ilikuwa haipo. Sasa kwa hivyo twataka hii Katiba itakayo undwa, ihakikishe kwamba kitu chochote ambacho kimepita katika Kenya na kwetu pia kifike. Siyo kwamba leo utolewe mapendekezo kwenye Katiba, kesho yafanyika Nairobi, yafanyika Mombasa, yafanyika Lamu na yafanyikayo kwetu ni tofauti. Likiwa jambo ni lakutufinya sisi, huja haraka maanake kwatakiwa leseni ya uvuvi, haraka tayari vitabu vimeshakuja twatakiwa leseni ya uvuvi. Lakini ikiwa ni msaada watakikana kusaidia wavuvi hausilikizwi. Utakoma njiani.

Sasa kwa hivyo ihakikishwe katika Katiba, kwamba mkondo huu ambao umehakikishwa kwamba wananchi wametoa mapendekezo ya Katiba ni kwamba irekebishwe kila kitu. Ikiwa kumetokea msaada, ikiwa kumetokea jambo lolote, kuhusu mwananchi wa Kenya, ikiwa ni mambo ya ulinzi yawe yatafikiriwa na yawe yatatelekelezwa kama kwa Kenya wengine. Isiwe jambo la nafuu litabakia huko, jambo kashikeni liko kule. Hiyo itakuwa si ubadilishaji wa Katiba. Kwa hayo machache Asante sana.

**Com. Mosonik:** Athman Abbas.

**Athman Abbas:** Asalaam Aleykum, Jina langu ni Athman Abbas. Mimi ningependa kuzungumzia kuhusu ulinzi. Ulinzi sisi

hatuna, kwa sababu hapa Kiunga na Shakani si mbali. Shakani na Kiunga tunaenda kwa miguu, halafu hapa Shakani hakuna ulinzi yelete, hakuna Kenya Army, hakuna askari hata Polisi, na hapa ndiyo border ya Kenya na Somalia, hakuna ulinzi wowote.

La pili ni kuhusu masomo, skuli inayo Walimu watano. Na hao Walimu watano, kuna class kumi na mbili, sasa hawa Walimu watano wakifundisha lower, wafundishe lower ama wafundishe upper? Hatujui wafundishe wapi.

Na lingine ni kuhusu ulinzi. Ulinzi hapa Kiunga Polisi wako juu, Game wako juu, Kenya Navy wako juu, hakuna ulinzi wowote uliojengwa chini, sasa sisi twawalinda wao ama wao watulinda sisi? Kwa sababu zote ziko juu, sisi ndio tuko chini na njia ya Somalia ndio hii yakwenda huko chini, kwa nini hawakujenga? Wakati wa siasa walikuja hapa, wakasema watatufanyia ulinzi wakaweka askari wa AP, waliwekwa pale Sekandi, halafu siasa ilipomalizika wamerudi mahali kwao sasa ulinzi huo uko wapi? Mimi sina mengi kwaherini.

**Com. Mosonik:** Je kuna mtu yelete mwingine ambaye yuko hapa hajajiandikisha na angependa kutoa maoni?

**Jamal Fankupi:** Kuna yelete ambaye alikuwa hajajiandikisha ana maoni, na sasa anataka kutoa maoni pengine alikuja kuchelewa ikawa washajiandikisha, ikiwa bado mtu aka na lolote na lakumkera asimame tafadhali.

**Com. Mosonik:** Na akiwa akifkiria Mwalimu Tajiri akasema hatubadilishi Katiba kwa ajili hatujui hiyo Katiba, akasema,

## Commotion

**Com. Mosonik:** Aseme kwanza wacha aseme, wacha akae, kaa tu, kaa tu useme kama umekaa.

**Maalim Faqi Ali Maalim:** Assalam Aleykum Warahmatullahi Wabarakatu waume kwa wake,

**Crowd:** Wa Aleykum salaam.

**Maalim Faqi Ali Maalim:** Hamjambo siyo? Mimi nasema hivi.

**Maalim Faqi Ali Maalim:** Hamjambo Siyo? Mimi nasema hivi,

**Com. Mosonik:** Sema Jina lako kwanza.

**Maalim Faqi Ali Maalim:** Jina langu mimi naitwa Faqi Maalim Faqi Ali Maalim, mimi nina mengi sana kwashauri mimi

kwanza naelewa mimi mwenyewe kwa shauri mi nilikuwa na fanya kazi ya safari , ni seaman, nilikuwa mimi niko wapi, kupakia petrol Libya nilikwenda kuteremsha mimi hailers back, hailers back nilipo kuwa nimekaa mara kanzo amekuja rais wetu wa Kenya (inaudible) Jomo Kenyatta, mara oh arabu Moi nikasema huyu ni muarabu kwa shauri huyu kiswahili hatusemi urongo, Swahili sema maanake liambiwalo liko liko si kanushe si urongo sikia bwana ndio nikamuita mimi nkamuita mwarabu, na jina ingine mimi namuita somo, mimi nasema ndugu yangu kwa dhihaka hapa mjini? Semeni, mimi hapa mjini nafuatwa maana tuseme mimi madirisha niki tungia, nishaharibu mimi mtoto wa kiume, nishaharibu mtoto wa kike mimi hapa, nishatembea na mwanamke hata mara moya si ati mwezi moja wala wiki moja, mara moja na mtu maanake ikiwa huyu mwanamke atoe usuhuda wake hapa ni mimi si nipigwe rasasi.

Na mimi nitazungumza ukweli, Serikali inifunge au inipige risasi lakini yale maneno nitaka yozungumza mimi waturongo halafu wanipige rasasi au wanifunge maisha, wasikia.

Jambo la kwanza mimi nasema hivi mimi ni lugha shauri kiswahili mimi ni lugha yangu, na kiswahili kilichoundwa hapa Kiunga (inaudible) si Kiswahili hicho maana Kiunga ni kuunga, Kiunga ndio uliounga maanake tuseme hicho. Kiswahili haikupelekwa na Kenyatta huko Zaire wala huko Kigali wala huko wapi isipokuwa waliopeleka ni wangwana na watoto wao kike na wale Warenco basi walipotoka hapa mjini wakikimbia ile aibu, walipoenda zao ndio kiswahili kikaenea ndio Kiunga ikaunga wasikia. Kiswahili kimeenea hapa maanake hii Kenya tuseme maana kushauri nini, hii Kenya yenyewe watu wa Kenya wote ni waswahili kwa shauri nini sisi wenyewe tumefundisha wale ma mvita na kusudi yakufundisha ma mvita alikuja yule mwana ngomeni akikaa kule ngomeni. Ilikuwa zamani sisi Bajuni tuna miko ambapo mwanamke hataki kusikiwa sauti yake, asili ya kukaa ngomeni asiuke sauti yake, lakini mwana ngomeni ndiyo akaja hapa akaja kwa babu yangu mimi mwenyewe kisha (inaudible) ambako nie na avia yangu na (inaudible) ya babu yangu, wasikia? Akasema nini tumefunga undugu sisi na wale ma mvita basi wafundisheni kiswahili, tukawafundisha Swahili lakini kuwa fundisha Swahili hawezi kufundishwa chote nikaa mimi na sikia masikio, masikio, miaka mingi sana wasikia hebu ulizeni kama yule kwamba anaitwa Nassiri (inaudible) masikio.

**Com: Mosonik:** Tafadhalii kuna mtu yejote mwininge, please, wacha mzee ninauliza kuna mtu mwininge yejote angependa kutoa maoni? Nilitaka tu kusema Mwalimu Tajiri akasema tuko kwa harakati za kuunda Katiba siyo kubadilisha, na vile amesema ni ukweli kwa ajili mukiona dibaji ya kijitabu hiki, kimeandikwa na Tume, mwenyekiti wa Tume Prof. Ghai, ameyatumia maneno tafauti tafauti kutaja tukifanya nini. Kwanza Tume inaitwa Tume Yakurekebisha Katiba ya Kenya, kurekebisha halafu akiandika dibaji, anasema “utengenezaji wa Katiba ni tukio muhimu,” kutengeneza, kurekebisha, kutengeneza, halafu anaendelea kusema hali “hii ya mageuzi ya Katiba kugeuza Katiba” halafu mwishowe akasema “nawatakieni heri katika uundaji wa Katiba,” kuunda vile mzee huyo alisema kwa hivyo kama ni kuunda, kubadilisha, kurekebisha, kugeuza na khadhalika inategemea sisi wenyewe raia.

Maoni yale yenu yote mmeyasema tutayachukua na tulinganishe na wa Kenya wengine wote. Halafu tukubaliane kama

kwamba, kulingana na maoni ya raia Katiba mpya ni lazima iwe hivi. Sasa mwishowe mtakata shauri tulitengeza, ama kugeuza ama kubadilisha ama kuunda. Ikiwa imekuwa tayari, itarudishwa kwenu kwa muda wa pengine mwezi moja ama miezi miwili kutakuwa tena na masomo ya uraia. Wakati ule mtaangalia hiyo Katiba mpya mjadiliane ni kama ile ya zamani tumerudisha, ama tumerekebisha ama tumegeuza ama tumetengeza ama nini, na mtoe tena maoni yenu ndio wajumbe wenu kutoka sehemu hii waende kwa mkutano mkuu wa taifa na wataje tena maoni yenu ya mwisho yakuingiza kwa hiyo Katiba kwa hivyo tumefurahi leo tumefika kwenu na tulikuwa tunafikiria kwa ajili hakuna watu wengine wanataka kutoa maoni pengine tuta achana ndio watu waende kwa Swala mapema. Kabla ya hapo pengine nani angependa kusema, Chief tutampatia, atufungie, kwanza Chief atufungie halafu tutaombewa na tutasema asante sana na kwaheri Bw. Chief sema.

**Jamal Fankupi:** Commissioner Korir, na wenzako ambao asubuhi hii umekua mwenye kiti wa kikao hiki, na wananchi wale ambao tumekuwa nao asubuhi hii mpaka sasa, leo ikiwa ni Ijumaa, kwa kutoa maoni na nyinyi mkayapokea kwa maandishi na kwa kurekodi pia vile vile hatuna budi kuwaregeshea shukran, Tume hii kwa kuweza kufika mpaka hapa Kiunga. Kwani kuna Tume nyingi ambazo zimeundwa Kenya hii kuchunguza au kubadilisha au kuunda mambo tofauti tofauti, laikini zote hizi, kati ya Tume zile ambazo zimewahi kuundwa, hakuna Tume ambayo imeweza kufika Kiunga isispokuwa Tume hii. Na hii ikiwa ni Tume ya kwanza, hii ikiwa ni safari ya pili safari ya kwanza ilikuwa ni mwezi uliopita tukiwa na Prof. Idha na Dr. Mohamed ambao walifika hapa na kulikuwa na maoni tofauti tofauti kutoka kwa wananchi. Kusema kweli kipindi kile kilikuwa kina moto zaidi, kwani watu walikuwa na hamu sana yakutaka kujua Katiba ni kitu gani au tumeitwa twende tukasikie nini.

Na kwa kipindi kile kifupi watu walipata elimu kiasi ya haja. Tukilingamanisha Kiunga Division na Division zinginezo, iko tofauti kubwa na tofauti kubwa ilioko hapa ni kwamba division zingine ama wilaya zingine watu walipata Civic Education kimbele, na wakawa wanafundishwa wakifundishwa kila siku. Kiunga mpaka kufika kina Dr. Mohamed na Prof. Idha ilikuwa hakuna Civic Education ya aina ye yeyote ambayo ulifanywa hapa. Na tungepata maoni mengi sana kutoka kwa wananchi wa Kiunga kama wangkuwa wamefundishwa ile Civic Education na kuweza kuwaingia katika bongo zao kisawa sawa na kujua ni kitu gani watakacho kuja kukizungumzia.

Leo hi kumekuwa na maoni na maombi na urekebishihi kiasi fulani kutoka kwa wale

wote walo simama hapa. Hatusemi wale wote walo simama hapa wamekuja na kurekebisha Katiba irekebishwe namna hii na namna hii na namna hii. Utakuta kuna maombi. Kwa hivyo hii ni kuonyesha kwamba ile Civic Education haikuwafikia wananchi vivilyo, na vile inavyo pasa, itakikanavyo hawaipati, ndio sasa ikaangukia hapa. Imekuwa ni ku express zile shida zao, kuzieleza zile shida zao, laiti kama ingekuwa imewaingia kama kule kwingine munako toka watu wengi hawakupata nafasi yakuzungumza. Watu wameandikishwa majina na wakati hauruhusu kuzungumza.

Leo hii hapa watu wameandikishwa, wote wale waloandikishwa wamepata nafasi yakuzungumza nakuelezea kile wanacho stahili kukizungumzia. Kwa hali kama hii mimi ningonelea jambo lolote linapo toka kuhusiana na wananchi liweze kusambaza kiharaka iwezekavyo mpaka imfikie mwananchi alioko katika corner fulani mbali na wale walioko kati kati ili tuwe ni sawa sawa kabisa. Sio waambiwe hawa wako mbali mpakani huko mtu akiambiwa aende akafundishe, aseme Kiunga ni mbali siwezi kufika. Kwa hali kama hii itakuwa inaturegesha nyuma, lakini nina hakika kama na sisi tungkuwa tuko katika mstari wa mbele kama wale wenzetu wale walipata elimu kama hii, natumai leo hapa wengi sana wangeongea na wangetoa maoni tofauti tofauti, kwa sababu sisi tuliokuwa huku mbali ndio tunao hisi zile shida zilizo huku na tunaziona zaidi kuliko wale walioko mjini.

Wale maisha inawaenda siku zote sawa sawa na kila kitu chenda vizuri lakini kwetu sisi twahisi kila pahali kwa kila pembe, kwa kila upande tunajihisi. Kwa hivyo ma Bwana Kamishnas mimi ningeomba baada ya kukaa chini kama ulivyosema nakuleta yote haya pamoja ya Kenya nzima, halafu tutaregeshewa tena ili tutakapo kuregeshewa tena Kiunga isisahaulike na mtukumbuke mueke katika mstari wa mbele kabisa iwe ni ya kwanza. Ni afadhali kuanzia huku kumalizia kati kati kuliko kuanzia kati kati kumalizia pembedi.

Pindi ufikapo kati kati ya safari yako utajisikia kuchoka na utaona hapa ambapo nimefikia basi imetoshea. Lakini ukianzia pembedi utakuwa unakimbia kule unapotoka. Kwa hivyo tufanyiwe namna hiyo ili tusione kwamba tumetengwa na wananchi wengine wale walioko Kenya. Sote tuko sawa, otherwise tumeshukuru sana tena sana kwa kuja kwenu hapa na ni matumaini yangu kwamba haitokuwa ndio safari yenu ya mwisho, mutakuja tena na matumaini yangu kwamba tutaendelea kuwafundisha hawa pole pole ili waweze kufahamu ki sawa sawa zake ijapokuwa wakati utakuwa umepita sana.

Lakini kile mtakachokutuletea sasa pengine katika hali yakurekebisha na kukubaliana kutakuwa na maoni mengine tofauti. Kwa hayo machache na sema Asanteni sana kwa kuja na wananchi kwa kuja kusikiza na kutoa maoni yao pia vile vile hatuna ziada isipokuwa wakati wa Ijumaa umefika hatuna budi na kukomea hapa. Nyote tuliokuwa hapa Mwenyezi Mungu atujalie liwe ni Ijumaa la kheri na yale tuloyatoa hapa Mwenyezi Mungu aayajaliye yawe yatafika kule na yatatiliwa maanani sawa sawa, asanteni.

Pale ambapo tumekomea nikutia fat'haa na kuomba ili tuweze kufunga kikao hiki.

**The prayer was said in Arabic and the meeting closed at 12.10**

**&&&&&&&&&&&&&**